

MAENDELEO

Mawaziri watatu wazindua mradi mkubwa wa kilimo

Mradi huo ulianza tangu mwaka 2005, utagharimu Sh.1 trilioni na unatekelezwa katika Wilaya ya Bagamoyo.

Elias Msuya, Mwananchi

Bagamoyo. Mawaziri watatu wakiongozwa na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mhandisi Christopher Chiza juzi walizindua Mradi wa Kilimo cha Miwa unatekelezwa na Kampuni ya Agro EcoEnergy (T) Ltd, utakaogharimu Sh.1trilioni wilayani Bagamoyo Mkoa wa Pwani.

Mbali na Chiza, mawaziri wengine waliohudhuria walikuwa ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambaye pia ni Mbunge wa Bagamoyo, Dk. Shukuru Kawambwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Profesa Anna Tibaijuka.

Akizungumza katika sherehe za uzinduzi wa mradi huo, katika Kijiji cha Kigongoni wilayani humo, mwenyekiti wa Agro Ecoenergy, Per Carstedt alisema mradi huo ulianza tangu mwaka 2005 na sasa umedhamiria kuzalisha sukari na



"Mimi sikuja kuweka jiwe la msingi hapa, ni lazima tumlete mtu mzito kabisa tena 'Champion' wa Kilimo Kwanza. Nitamwomba yeye ndiye aweke jiwe la msingi,"

Christopher Chiza

umeme kwa manufaa ya Watanania.

"Leo ni furaha kubwa kuzindua shughuli zetu tangu tulipoanza maandalizi mwaka 2005, Mradi huu ni mkubwa kuliko yote Afrika Mashariki kwani utagharimu Sh1trilioni. Tunategemea kuanza

kuzalisha sukari baada ya miaka miwili," alisema Carstedt.

Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Christopher Chiza alisema mbali na kuzindua mradi huo, bado atamwalika Rais Jakaya Kikwete auzindue rasmi.

Aliongeza kuwa mradi huo umechukua muda mrefu kutokana na jitihada za Serikali na mwekezaji kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uwekezaji na changamoto za ardhi.

Waziri Tibaijuka aliwahakikishia wananchi wa Bagamoyo kuwa mradi huo utakuwa na manufaa kwao.

Profesa Tibaijuka alisema licha ya shamba hilo kuwa na ukubwa wa hekta 20,365 bado ametoa hekta 2000 kutoka Kijiji cha Fukayose ili kuongeza.

Wengine waliohudhuria ni Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mwanatumu Mahiza, Balozi wa Sweden, Lennarth Hjelmaker, Mkurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), Julieth Rugeiyamu, Katibu Mkuu Mstafu, Peniel Lymo na Mwenyekiti wa Bodi ya Mwananchi Communications Ltd, Zuhura Muro.